# MKATABA WA MATUMIZI YA ARDHI
# KIJIJI CHA ENGARESERO NA KAMPUNI YA
# LEONOTIS ADVENTURE LIMITED
# KWA AWAMO YA PILI

1 January 2018

Mkataba huu umewezeshwa na umeeandaliwa na :-
Ujamaa Community Resource Trust
P.O Box 15111,
ARUSHA - TANZANIA

Kisau and Company Limited
P.O Box 6251
ARUSHA – TANZANIA

Mkataba huu unatiwa saini leo tarehe 31 jan, 2018 kati ya kampuni Leonotis Adventure Limited yenye anuani P.O Box 14342 Arusha Tanzania na Halmashauri ya kijijicha Engaresero yenye anuani S.L.P 1 Loliondo Arusha . Tanzania kwa kizingatia mamlaka ya Halmashauri ya kijiji ya kusimamia na kutawala ardhi yote iliyoko ndani ya mipaka ya kijiji kwa kulingana na kifungu Na. 8 cha sheria ya ardhi ya vijiji Namba 5 ya 1999; na uwezo wa kisheria kuingia katika mikataba yoyote baada ya kupata idhini ya mkutano mkuu wa kijiji kwa mjibu wa vifungu Namba 26 na 142 vya sheria ya serikali za mitaa (mamlaka ya wilaya ) Namba 7 ya 1982; na baada ya Halmashauri ya kijiji kupewa na mkutano mkuu wa kijiji cha Engaresero na kutenga na kukodisha eneo la kampuni ya Leonotis Adventure LTD kwaajili ya matumizi ya biashara ya utalii tu, kulingana na mipaka kamili ya kijiji kama ilivyoelekezwa na Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro katika kiambatanisho cha 1

Wakati wowote, kampuni kupitia maamuzi ya pamoja ya bodi ya wajumbe wa kampuni inaweza kupeleka maombi kwa msajili wa makampuni kubadili jina la kampuni iwapo badiliko hilo itapelekea kuboreshwa kwa malengo ya kampuni bila kuadhiri makubaliano ya kijiji na kampuni.

Malengo ya mkataba huu ni:

1) Kuhakiksha kuwa uchumi na maslahi ya kijamii ya pande zote mbili zinazohusika yatakuwepo na kutambulika na kuhakikisha kuwa shughuli za kitalii zitakazofanyika katika kijiji cha Engaresero zinaleta Mapato na faida kwa pande zote mbili,na kupunguza vitendo vyovyote amabvyo vinaweza kuharibu mazingira na mila na desturi za jamii husika .

2) Kukuza moyo wa ushirikiano kati ya leonotis adventure na jamii ya kijiji cha Engaresero kwa kushirikiana katika ujuzi,maarifa na maslahi ya kifedha ili kuhakikisha kuwa ushirikiano huo unadumishwa.

3) Katika kuendeleza mahusiano kati ya kampuni ya leonotis Adventure na kijiji cha Engaresero,razilimali za fedha zitalenga katika kutoa huduma za kijamii na Elimu ya Secondary kwa wanafunzi waotokea kijiji cha Engaresero . hivyo basi pande zote mbili zinaingia katika maktaba wa kuazisha shughuli za biashara ya kitalii ndani ya ardhi au kijiji kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika mkataba huu kama ifuatavyo;

<u>ENEO LA MAKUBALIANO KWA SHUGHULI ZA KITALII</u>

4) Halmashauri ya kijij cha Engaresero itatoa eneo litakalotumika kwa shughuli za kitalii lenye ukubwa wa Ekari 10 kwa kampuni pekee ya leonotis Adventure katika Engong Esidai kujengea kambi za

hema ya msimu na sio kwa matumizi mengine kulingana na mkataba huu ,eneo hii itakuwa likirejewa kama eneo la makubaliano.

a) Kijiji cha Engaresero pia imekubali kutoa eneo(buffer zone) linalizunguka Eneo la makubaliano lenye umbali wa mita 1000 kwa upande zote kuanzia katikati la eneo la makubaliano(GPS; S 02 35.870 E 35.55.157) Kampuni ya leonotis Adventure itakuwa na haki ya kipekee za kufanya shughuli zote eneo la makubaliano pamoja na 'bufferzone'.
b) Halmashauri ya kijiji cha Engaresero itahakikisha kwamba hakuna uingiliaji holela katika eneo la makubaliano kwa muda wa mkataba huu,ili kulinda haki za kipekee za kampuni za uwekezaji ya leonotis adventure . wanyama na mifugo wanaruhusiwa kula ndani ya (bufferzone) lakini ni marufuku kuwalisha kambini.

5) Kampuni ya uwekezaji ya leonotis adventure inaweza kutumia maeneo mengine ya kijiji kwa shughuli za kitalii kulingana na sheria ndogo ya kijiji kwa kufuata mipango yeyote ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa kushirikiana na wadau wengine.

6) Kampuni ya leonotis adventure hatatumia maeneo ya kijiji kwa matumizi mengine yoyote kinyume na mkataba huu na itafanyika kinachowezekana ili kuzuia kutokea uharibifu wowote wa kimazingira katika eneo la makubaliano na lisilo la makubaliano utakaosababishashwa na kampuni na watumishi wake.

7) Kampuni ya Leonotis Adventure itaajiri na itawezesha wanakijiji wenye uwezo na zifa zinazoitajika kufanya kazi zifuatazo;

a) Sio zaidi ya walinzi wanne wakati kuna wageni wengine kambini na mlinzi mmoja wakati hakuna wageni kambini, pia wasijishughulishe na makampuni mengine.

b) Wafanya kazi wote wa Leonotis Adventure wanaitajika kuingia mkataba na kampuni.( watalipishwa NSSF,PAYE, Skill & development levy)

c) Wafanyakazi watapewa onyo tatu kwa barua ,kabla ya kuwachishwa kazi. Wafanyakazi watakaefanya vitendo vibaya wataachishwa kazi hapo hapo kwa barua (1) tuu,vitendo vibaya kama uwizi ,ujambazi,ujangili,na uaribifu wa kambi na mazingira .kijiji zitapa nakala za hizi barua.

8) Kijiji cha Engaresero kitalipwa kodi ya ardhi kwa dolla za kimarekani elfu moja (1000) kwa mwaka kwaajili la eneo la makubaliano,na dolla 15 (USD 15) Kama malipo ya kichwa cha kila mtalii atakayelala katika kambi kwa kila siku moja katika eneo la makubaiano Na malipo ya dolla kumi na tano (USD 15) kwaajili ya malipo ya wildlife Division( WD), Malipo ya dolla 15 hayatawahusu wafanyakazi wa kampuni wa Leonotis Adventure. Watoto wenye miaka isiozidi 12 watalipa dola kumi (USD 10) , Familia na rafiki wa wakurugenzi watalipa kumi(USD 10).

9) **MALIPO YATAFANYIKA KAMA IFUATAVYO;**

a) Malipo ya kichwa cha kila mgeni kwa siku yatalipwa baada miezi tatu , kulinga na na idadi ya wageni.

b) Malipo yatafanyika kwa kupelaka hundi ya malipo katika akaunti ya benki ya kijiji cha Engaresero itakayofunguliwa kwa madhumuni hayo.

c) Stakabadhi za kuwekewa fedha zitumwa kwa halmashauri ya kijiji cha Engaresero mapema baada kuweka fedha benki.stakabadhi hiyo iwe imepokelewa na halmashauri ya kijiji kabla ya mwisho wa miezi tatu zinazofuata.

d) Kijiji kitoa nakala ya ukaguzi wa mahesabu 'audit' iliyofanywa na Halmashauri za kila mwaka. Kampuni itawapa kijiji booking sheet na bank deposit slip.

**USIMAMIZI WA MKATABA**

10) Halmashauri ya kijiji cha Engaresero ina haki ya kutembelea eneo la makubaliano na kufanya ukaguzi baada ya kutoa taarifa ya kufanya hivyo kwa muda ya masaa 24 , pia ina haki ya kugagua vitabu vya kumbukumbu vya wageni waliolala kambini na muda wa kufanya ukaguzi huo utapangwa kwa makubaliano kati ya kampuni na halmashauri ya kijijiili wageni wasipate usumbufu.

11) Kulingana na utaratibu uliyomo katika sheria ndongondogo za kijiji cha Engaresero , halimashauri ya kijiji ina wajibika kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa mkutano mkuu wa kijiji baada ya miezi mitatu na kualika uongozi wa kampuni ya Leonotis A dventure kuhudhuria mkutano huu ili kusaidia kutoa taarifa ya mapato na matumizi na uhusiano wa kitalii kwa wanakijijji kulinga na makumbaliano ya mkataba.

a) Uongozi wa kampuni la Leonotis Adventure na kamati ya mazingira na utalii wa kijiji cha Engareserozitakutana kama inavyotakiwa ili kujadili maswala inayohusu mazingira na Utalii za Katika kijiji na masuala yatokanayo na usimamizi wa mkataba huu.

b) Iwapo pande zote mbili itashindwa au itavunja masharti ya mkataba huu,hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya watakahusika.

c) Mgogoro utakaotokana na mkataba huu vitasuluhushwa katika vikao vilivyopangwa kukutana mara moja baada ya miezi mitatu. Mgogoro yote ni lazima itatuliwe kwa njia za kimahakama.

d) Utaratibu wa tarehe za vikao hivyo itapangwa na pande zote mbilina kuhakikisha utaratibu huo unafutwa.

12) Kampuni ya Leonotis Adventure na kijiji cha Engaresero zitashirikiana na kuakisha kwamba madhara ya aina mbaya (hasi) yatokanayo na biashara za kitalii yatapunguzwa kadri itakavyo wezekana ili yasilete madhara kwa jamii na wataunda na kutayarisha mipango na taratibu za usimamizi endelevu wa shughuli za kiatlii katika kijiji.

13) Mawasiliano yoyote ya kimaandishi yatafanyika kwa mjibu wa mkataba huu,yatafanyika kwa njia zinazoaminika kama kumia saduku la posta au kwa njia ya kusainisha katika kijitabu husika (DISPATCH BOOK)

**14) MUDA WA MKATABA HUU**

a) mkataba huu utadumu kwa muda miaka kumi kuanzia tarehe ya January 2018 baada kutiwa sahihi kwa upande zote .mkataba huu waweza kuendelezwa kwa kipindi kingine.
b) Katika kipindi cha miaka minne pande zote mbili zitakaa na kutadhimini mwenendio wa mkataba.

15) Baada ya awamu ya miaka kumi wa mkataba kama pande zote mbili zimetimiza masharti yaliyoko katika mkataba huu awamu ya tatu ya mkataba wa miaka kumi utaridhiwa

16) Awamu ya pili ya miaka kumi ada ya kichwa ya kila mtalii itajadiliwa na itaongezeka kulingana na makubaliano ya pande zote husika .

17) Mkataba huu unaweza kufanyiwa marekebisho kwa makubaliano baina ya pande zote mbili kila inapoonekana kuwa kuna sababu ya kufanya hivyo na marekebisho hayo lazima yaambatanishwe na mkataba huu.

SHERIA ITAKAYOONGOZA MKATABA HUU

18) Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na sheria za Tanzania bara. Mkataba huu tumeuandika kwa pamoja na tumesoma na kuyelewa. Tunatia sahihi yetu na muhuri hapa chini kuonyesha makubaliano yetu.

WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ENGARESERO

| S/NO | JINA | WADHIFA | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 1 | SAIMON ZEPHANIA | MJUMBE | |
| 2 | PARMITORO NDIRIMA | MJUMBE | |
| 3 | EMMANUEL SIMANDE | MJUMBE | |
| 4 | WILIAM MEPISHANA | MJUMBE | |
| 5 | ELIAS NDURWAY | MJUMBE | |
| 6 | LANJOO KAKANYI | MJUMBE | |
| 7 | PARKEPU NATISILE | MJUMBE | |
| 8 | YONA KOROMO | MJUMBE | |
| 9 | SAMWEL KATANGA | MJUMBE | |
| 10 | ESUPAT NGOYIASI | MJUMBE | |
| 11 | NORETET OLOJU | MJUMBE | |
| 12 | SOPHIA NDAKAR | MJUMBE | |
| 13 | NADUTARI NASIPU | MJUMBE | |
| 14 | TIYA OTE | MJUMBE | |
| 15 | NOONDOMON NDIONO | MJUMBE | |
| 16 | MARIA JACKSON | MJUMBE | |
| 17 | NOLTETAIN OLESONDO | MJUMBE | |
| 18 | KEEMBWA KITINA | MJUMBE | |
| 19 | PHILIMON MSUYA | MJUMBE | |
| 20 | SAYORE SURUPE | MJUMBE | |
| 21 | ANNA ABRAHAMU | MJUMBE | |
| 22 | YOHANA SEPER | MJUMBE | |
| 23 | NANYAKWA TOONDE | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23 | NANYAKWA TOONDE | MJUMBE | |

YOHANA M. LAIZER **MWENYEKITI** ..........................................................................

THOMAS L. LAIZER **AFISA MTENDAJI** ....................................................................

**SHAHIDI**

IBRAHIM SAKAY **DIWANI KATA**..........................................................................

LASOI NARESHO **MTENDAJI WA KATA** .................................................................

IPANGA KIMAAY **MWANASHERIA WA KIJIJI** ...........................................................

**MBELE YA:**

**WAKILISHI WA KAMPUNI LA LEONOTIS ADVENTURE LTD**

AKE LINDSTROM **DIRECTOR** ..........................................................................

NANGINI LUKUMAY **DIRECTOR**..........................................................................

PETER LINDSTROM **DIRECTOR**..........................................................................